



## TAARIFA KWA UMMA

### MWENENDO WA KILICHOKUWA KIMBUNGA “JOBO”

Dar es Salaam, 25 Aprili 2021 Alfajiri:

Taarifa hii inahuisha taarifa ya kimbunga hafifu “Jobo” iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) jana mchana tarehe 24/04/2021. Mwenendo wa kimbunga hafifu “Jobo” unaonesha kuwa katika kipindi cha saa sita zilizopita “Jobo” imepoteza nguvu yake wakati kikiingia nchi kavu kusini mwa mkoa wa Pwani na Dar Es Salaam usiku wa tarehe 24/04/2021. Hali hii ilisababishwa na kuendelea kuimarika kwa upopo kinzani katika mwelekeo wa kimbunga hicho.

Aidha, mawingu ya mvua yaliyokuwa yakiambatana na kimbunga hicho yamesambaa baharini karibu na maeneo ya kusini mwa pwani ya Tanzania na Msumbiji.

Hivyo kwa sasa, kimbunga hafifu “Jobo” hakipo katika nchi yetu na hakuna madhara ya moja kwa moja yanayotarajiwa. Hata hivyo masalia ya mawingu yanayoambatana na kilichokuwa kimbunga “Jobo” yanaweza kusababisha mvua katiaka baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani.

**USHAURI: Wananchi wanashauriwa kuendelea kufuatilia na kuzingatia taarifa za utabiri kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania pamoja na maelekezo na miongozo inayotolewa na mamlaka husika.**

**Imetolewa na:**

**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Morogoro Rd, Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3  
S.L.P. 3056, Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8

Barua pepe: [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz), Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

(IMETHIBITISHWA - ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)

105A - 09/19